



JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

TUME YA TAIFA YA UCHAGUZI



TAARIFA KWA UMMA

KUHUSU UTEUZI WA WAGOMBEA UBUNGE KATIKA MAJIMBO
MANNE NA UDIWANI KATIKA KATA 47 ZA TANZANIA BARA

Tarehe 3 Novemba mwaka 2018, Tume ilitangaza kuwa ni siku ya uteuzi wa wagombea katika Uchaguzi mdogo wa Ubunge katika Majimbo ya Babati Mjini, Ukerewe, Simanjiro na Serengeti na Udiwani katika Kata **Arobaini na saba (47)** za Tanzania Bara. Uteuzi huo ulifanyika kama ilivyopangwa.

Katika Majimbo hayo **manne (4)** Vyama (6) vya Siasa vilishiriki kwa wanachama wao **Kumi na tatu (13)** kuchukua fomu za uteuzi. Vyama hivyo ni AAFP, CCM, CUF, NCCR - Mageuzi, NRA na UDP.

Katika Kata hizo **Arobaini na saba (47)**, Vyama kumi na nne (14) vya Siasa vilishiriki ambapo wanachama wao **Mia moja na mbili (102)** walichukua Fomu za Uteuzi, vyama hivyo ni AAFP, ACT - Wazalendo, ADC, CCK, CCM, CHADEMA, CUF, DEMOKRASIA MAKINI, NCCR - Mageuzi, NRA, SAU, TLP, UDP na UPDP.

Hadi muda wa mwisho wa uteuzi tarehe 3 Novemba, 2018 saa 10: 00 jioni jumla ya Wagombea **wanne (4)** wa Ubunge kutoka CCM waliteuliwa na hivyo kutangazwa kuwa wamepita bila kupingwa, hii ni kwa mujibu wa kifungu cha 44 cha Sheria ya Taifa ya Uchaguzi.

Kwa upande wa Udiwani katika kata 47, hadi muda wa mwisho wa Uteuzi tarehe 3 Novemba, 2018 saa 10.00 jioni kati ya wanachama (102) waliochukua fomu za uteuzi ni Wanachama 73 walirejesha fomu na kuteuliwa kuwa wagombea udiwani. Wanachama wengine 29 waliokuwa wamechukua fomu za uteuzi hawakuteuliwa kuwa wagombea kutokana na sababu mbalimbali ikiwemo kushindwa kurejesha fomu za uteuzi, kutojaza fomu za uteuzi kwa usahihi, kutosaini fomu ya kuheshimu na kuzingatia Maadili ya uchaguzi na kukosa sifa za kugombea udiwani kwa mujibu wa sheria.

Jumla ya wagombea 15 wa nafasi ya Udiwani waliwekewa pingamizi kwa Msimamizi wa Uchaguzi na hivyo kupelekea wagombea 9 kuenguliwa kutoka katika orodha ya wagombea wa nafasi ya Udiwani.

Tume ya Taifa ya Uchaguzi ilipokea Rufaa 2 kutoka kwa wagombea Udiwani wa Kata ya Muhinda iliyopo Halmashauri ya Wilaya Buhigwe na Kata ya Mnyamani iliyopo katika Halmashauri ya Manispaa ya Ilala. Katika rufaa hizo mbili wagombea walikata rufaa kupinga maamuzi ya Wasimamizi wa Uchaguzi kuwaondoa katika kugombea udiwani.

Tume katika kikao chake kilichofanyika leo tarehe 9 Novemba 2018 kimetoa maamuzi kama ifuatavyo:-

Kwanza, Tume imekubali rufaa moja ya mgombea Udiwani wa CUF katika Kata ya Muhinda Halmashauri ya Wilaya ya Buhigwe na hivyo kumrudisha kugombea nafasi hiyo.

Pili, Tume imekubaliana na maamuzi ya Msimamizi wa Uchaguzi katika Kata ya Mnyamani iliyopo Halmashauri ya Manispaa ya Ilala ya kumuondoa mgombea wa CUF katika orodha ya wagombea na hivyo Mgombea kuendelea kuenguliwa kugombea Udiwani.

Katika Uteuzi huu wa Udiwani katika Kata **Arobaini na saba (47)** jumla ya Wagombea udiwani katika **Kata Arobaini na Moja (41)** wamepita bila kupingwa, na hivyo kata Sita (6) ndio zitakazofanya uchaguzi hapo tarehe 2 Desemba 2018, kata hizo ni **Nkoanekoli** iliyopo Halmashauri ya Wilaya ya Meru, **Kivinje/Singino, Mteja, Somanga, Mitole** zote katika Halmashauri ya Kilwa na Kata ya **Butimba** katika Halmashauri ya Wilaya ya Bunda.

Kampeni za uchaguzi zimeshaanza kwa mujibu wa ratiba ya uchaguzi na zitaendelea hadi tarehe 1 Desemba 2018 ikiwa ni siku moja kabla ya siku ya Uchaguzi.

Tume ya Taifa ya Uchaguzi inavikumbusha vyama vya siasa na wagombea wao kuwa vinapaswa kuheshimu Maadili ya Uchaguzi wa Rais, Wabunge na Madiwani ya mwaka 2015, wakati wote wa kampeni na hata Siku ya Uchaguzi

Taarifa zaidi kuhusu walioteuliwa inapatikana kwenye tovuti ya Tume ya Taifa ya Uchaguzi ya www.nec.go.tz na Ofisi za Tume Makao Makuu.

Imetolewa leo tarehe 9 Novemba, 2018.

Giveness S. Aswile
KAIMU MKURUGENZI WAUCHAGUZI